



### **Mkuu wa Wilaya Rahabu Mwagisa ziarani kujionea maendeleo ya miradi fedha za uviko 19**

Wananchi wilayani Manyoni wametakiwa kuacha kukaa majumbani na vijiweni badala yake wajitokeze na kuongeza nguvu kazi katika zoezi la ujenzi wa madarasa unaondelea wilayani humo

Wito huo umetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Manyoni Rahabu Mwagisa alipotembelea miradi hiyo ya ujenzi wa madarasa ikiwa sehemu ya ziara yake ya kutembelea miradi hiyo na kujionea ilipofikia na kuhamasisha wananchi kujitolea ili mirad hiyo iweze kukamilika kulingana na maelekezo ya Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Samia Suluu Hassan.

Mwagisa amesema kuwa kila mwananchi ndani ya Wilaya ya Manyoni maeneo ambayo yamepata fedha za mradi anatakiwa kutoka kuongeza nguvu kazi kwani madarasa yanatakiwa kukamilika mapema kabla ya desemba 10,2021

“Nimesema kote nilikopita ndani ya wilaya wananchi tutoke tushiriki kuongeza nguvu kazi tusaidie viongozi ili madarasa yakamilike ndugu zangu tutambue kuwa madarasa haya ni faida ya Watoto wetu tumuunge mkono Rais wetu mama Samia kwa kutuletea fedha za ujenzi basi sasa tukimbizane na muda tujitokeze jamani.”alisema Mwagisa.



### **Afisa Tarafa wa tarafa ya kintinku akitoa utambulisho baada ya timu ya Mkuu wa Wilaya kuwasili kata ya makanda**



**Dc Mwagisa akielekeza jambo**



**Ukaguzi ukiendelea katika kitongoji cha igose**



**Muonekano wa ujenzi wa madarasa shule ya sekondari ngaiti**



**Shule ya sekondari ngaiti ujenzi ukiendelea**



**Kintinku sekondari wameanza kujenga msingi**



**Ujenzi wa madarsa shule shikizi waraka kintinku**

